**Mtihani wa Mwisho wa Muhula wa Pili Mwaka wa 2020**
**102/3**
**Kidato cha 3**
**Tarehe:** ..............................
**Alama: 80**
**Muda: Saa mbili unusu**

JINA: ..........................................................................................................................................................................
MKONDO: ........................... NYUMBA: .................................
JUMLA YA ALAMA: .......... / 80 = ....... %

**MAAGIZO:**

1. Mtihani huu una kurasa nane zilizopigwa chapa.
2. Jibu maswali manne tu.
3. Swali la kwanza ni la lazima.
4. Chagua mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia.
5. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| A | 20 | |
| B | 20 | |
| C | 20 | |
| D | 20 | |
| Jumla (Maswali Manne) | 80 | |

**SEBEMU YA A: TAMTHILIA**

**P. Kea: Kigogo**

1.
   a. Jadili mbinu kumi ambazo Wanasagamoyo wanatumia kupigana na utawala

      dhalimu. (alama 10)

   b. Eleza jinsi mbinu rejeshi ilivyotumiwa kukuza vipengele vifuatavyo katika tamthilia hii.

      i. Maudhui (alama 5)

      ii. Wahusika (alama 5)

**SEHEMU B: HADITHI FUPI**

Jibu swali la 2 au la 3

**A. Chokocho na D. Kayanda (Wah):** Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

Kenna Wasike. "Mapenzi ya Kifaurongo"

2.
   a. ."Penzi lenu na nani?.... Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Potelea mbali mkate wee!"
   b. Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
   c. Taja na ufafanue mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika

      dondoo hili. (alama 4)

   d. Onyesha vile maudhui ya utabaka yanavyojitokeza katika

      hadithi nzima. (alama 6)

   e. Eleza sifa sita za mzugumzaji kwenye dondoo. (alama 6)

3.
   a. Onyesha jinsi unafiki unavyoshughulikiwa katika hadithi, "Shogake Dada

      ana Ndevu." (alama 8)

   b. Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 12)

"Bi. Hamida alitunga donge kifuani mwake. Na donge likaja juu. Likampanda na kumsakama kooni. Kweli? Uongo? Kweli au uongo yale maneno ya binti yake?

Labda kweli anamfikiria mambo mabaya binti yake tu. Labda kweli dhana yake ni mbovu. Bi. Hamida alichanganyikiwa na mambo.

Alivutwa huku na huku na nafsi yake yenye chagizo. Upande mmoja sauti yake ya ndani ilikuwa inamtetea Safia, na upande wa pili wa nafsi yake ilikuwa ikimshuku Safia; na sauti zake zote mbili hizo zimo ndani ya kiwiliwili chake zinamvuta yeye mtu mmoja, Bi. Hamida. Hatimaye hakutambua afanye nini."

**SEHEMU C: USHAIRI**

Jibu swali la 4 au la 5.

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Lilipo lile banda, lile pale,

Kuna tuja kakonda, kwa uwele,

Wala siye kupenda, hiyo ndwele,

Ndwele ya kutishwa!

Ni ndwele ya kutengwa, penye haki,

Uwele wa kusutwa, pasi haki,

Ugonjwa kupuuzwa, na miliki,

Ndwele ya kutwishwa!

Mwiliwe kawa sugu,

viwandani, Uso una kunyugu,

ziso fani, Ujira wake ndugu,

ni mapeni, Ndwele ya kutwishwa!

Na homa akipatwa, maishani,

Kwa tiba apuuzwa, kama nyani,

Hajulikani kuwa, yeye nani,

Ndwele ya kutwishwa!

Ana chawa nyweleni, ona dhiki,

Na kunguni nguoni, ahiliki,

Funza na miguuni, wamesaki,

Ndwele ya kutwishwa!

Bado yuasubiri, kisimati,

Dhiki yake kutiri, 'we tamati

Ndipo iwe sururi, ya kidhati

Nyota yake, ni nyota ya huzuni.

(K.Wamitila)

a. Fafanua kwa kutoa hoja sita kutoka kwenye shairi, jinsi nyota ya anayerejele wa ni ya huzuni. (alama 6)

b. Eleza muundo wa shairi hili. (alama 3)

c. Bainisha aina zifuatazo za uhuru wa kishairi katika shairi: (alama 4)

   i. Inkisari

   ii. Kufinyanga sarufi

d. Eleza tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

e. Eleza sifa mbili za anayelengwa katika shairi hili kwa kurejelea ubeti wa mwisho. (alama 2)

f. Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 2)

5. Soma Shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Kama akili si mali, maskini na tajiri

Wangali moja sampuli, asikuwepo fakiri

Na hangekuwa na mali, mwenye bila kufikiri

Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Ukeshapo kwa fikra, ni kwa wingi wa akili
Kuwaza kigaragara, una mengi si kalili
Na kuwa una tambara, metajirika kwa hili
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Alokijenga kitanda, ana wingi wa akili
Hata asiwe na bunda, hamithili kwa akili
Hata naye paka nunda, pasipo akili hali
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Akili kweli ni mali, kwa kuteua vya mwozo
Singetumia akili, ungevila vya angamizo
Afya ikawa thakili, na kuhiliki mawazo
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Vipi gonjwa kikuganda, wawazia spitali?
Huachi ukawa ng'onda, ukanyauka muwili
Ugangani unakwenda, kutafuta afadhali,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Kama akili si mali, kusingekuwa na jela,
Kuwatenga kuwa mbali, wenye hiana na hila,
Kwa mbavu na ufidhuli, pamwe mbinu tolatola,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Tajiri na maskini wote wanayo akili,
Ni kuwa hayafanani, waliyonayo makali
Kabisa hawashibani, liwe lile au hili,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Kama akili si mali, 'singekuwa na hazina
Ya kudadisi mithali, na kumpinga yako mnna
Gani inadumu mali, kuliko huko kusana?
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

(T. Arege)

a. "Ufanisi wa binadamu hutegemea akili." Fafanua kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye shairi hili. (alama 6)

b. Andika mifano ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili: (alama 4)

    i. Sitiari
    ii. Tanakuzi
    iii. Swali la balagha
    iv. Kinaya

c. Eleza mbinu nne ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

d. Andika aina mbili za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

e. Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

Jibu swali la 6 au la 7.

6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Shangazi anambila

umewadia muda

wa kukiacha kiambo

cha Baba

Nende kujinasibisha

na ajinabi tusohusiana

kwa ngeu wala usaha

nache niwapendao

nache aila

nache matamanio

ya elimu kufuatiya.

Anambile shangazi

Hino ni neema

ela moyo wanirai

"Wajitia shemere", nami nauambia,

"Najua si utashi wangu"

ila hiari sina

kwani hivi ni faradhi

mitamba mepokelewa

na ami kwa furaha

kilobaki ni kuvuka

kizingiti hiki."

Kwaheri'i Mama, kwaheri wanuna.

a. Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 2)

b. Andika sifa mbili za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. (alama 2)

c. Eleza aina nyingine tatu za nyimbo. (alama 6)

d. Jadili umuhimu wa nyimbo katika jamii. (alama 10)

7. Linganisha na ulinganue fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 20)

**Mwisho wa mtihani.**